**HOTUBA YA MHESHIMIWA JOEL ARTHUR NANAUKA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MAENDELEO YA VIJANA KATIKA UFUNGUZI WA VIJANA PLATFORM KWA VIJANA WA VYUO VIKUU MKOA WA SINGIDA, TAREHE 12 FEBRUARI 2026 KATIKA UKUMBI WA CHUO CHA TIA KAMPASI YA SINGIDA.**

---

- Mhe. Halima Omary Dendego, Mkuu wa Mkoa wa Singida;
- Dkt. Kedmon Mapana, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana;
- Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida;
- Bw. Kaimu Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Kampasi ya Singida;
- Viongozi na Watumishi wa Ofisi ya Rais – maendeleo ya Vijana mliopo;
- Wawakilishi wa Taasisi za Umma na Binafsi mliopo;
- Viongozi Wawakilishi wa Vyuo mbalimbali vilivyopo katika Mkoa wa Singida;
- Viongozi wa Taasisi za Fedha (CRDB, NMB, UTT);
- Wadau wa maendeleo ya vijana mliopo;
- Ndugu vijana;
- Waandishi wa Habari;
- Mabibi na mabwana.

**Kazi na Utu, …**

Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutukutanisha hapa leo katika tukio hili muhimu la ufunguzi wa Vijana Platform kwa vijana wa Vyuo Vikuu na Vya Kati katika Mkoa wa Singida. Tukio hili ni sehemu ya jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita za kuhakikisha vijana wanashirikishwa kikamilifu katika ujenzi wa Taifa.

**Ndugu vijana,**

Napenda kutumia nafasi hii kutoa historia fupi kuhusu Vijana Platform. Jukwaa hili nililizinduliwa rasmi tarehe 10 Januari 2026 Mkoani Dar es Salaam. Uzinduzi huo uliashiria mwanzo wa mfumo mpya wa Serikali wa kuwasikiliza, kuwahusisha na kuwawezesha vijana katika masuala ya maendeleo, ajira, ujasiriamali, ubunifu na uongozi.

Vijana Platform ni jukwaa la kitaifa linalowaunganisha vijana kutoka makundi mbalimbali wakiwemo wanafunzi wa Vyuo Vikuu, Vyuo vya Kati, Vijana wasafirishaji (bodaboda na bajaj), Wafanyabiashara ndogo ndogo (Machinga), na vijana waliopo kwenye jamii wanaojishughulisha na shughuli mbalimbali—ili waweze kutoa mawazo, kushiriki katika majadiliano ya sera, kupata taarifa za fursa, na kushirikiana na Serikali na Wadau wengine katika kujenga mustakabali wao.

Malengo makuu ya Vijana Platform ni pamoja na:

1. Kuimarisha ushiriki wa vijana katika maamuzi na mipango ya maendeleo ya Taifa.
2. Kutoa jukwaa la mawasiliano ya moja kwa moja kati ya Serikali na vijana.
3. Kuunganisha vijana na fursa za ajira, ujasiriamali, ubunifu na teknolojia.
4. Kukuza uongozi, uzalendo na uwajibikaji miongoni mwa vijana.
5. Kuwezesha vijana kuwa sehemu ya suluhisho la changamoto zinazowakabili.

**Ndugu Vijana,**

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022**,** vijana wenye umri wa miaka 15–35 ni takribani milioni **20.6**, sawa na asilimia **34.4** ya wananchi wote. Hii inaonesha kuwa vijana ni nguvu kazi kubwa na msingi wa Maendeleo ya Taifa.

**Ndugu vijana,**

Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emanuel Nchimbi, Makamu wa Rais**,** na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lamerk Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao thabiti, maono makubwa na maelekezo mazuri wanayoendelea kuyatoa kwetu. Sisi katika Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana tunaendelea kuyatekeleza maelekezo hayo kwa weledi na ufanisi mkubwa**,** kwa lengo la kuwawezesha na kuwaendeleza vijana wa Taifa hili la Tanzania.

Ni katika dhamira hiyo, Mheshimiwa Rais ameonesha uongozi wa mfano kwa kuunda Wizara mpya ya Maendeleo ya Vijana chini ya Ofisi ya Rais, ili masuala ya vijana yapate uzito na uratibu wa karibu katika ngazi ya juu ya Serikali.

Sambamba na hilo, Mheshimiwa Rais aliahidi kutenga shilingi **bilioni 200** kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali kiuchumi. Fedha hizo zitagawanywa katika Wizara za kisekta ili ziweze kuwafikia Vijana katika sekta husika. Ofisi ya Rais imepewa jukumu la kusimamia na kuratibu jukumu hilo ili liweze kutekelezwa kwa ufanisi.

**Ndugu vijana,**

Wizara ya Maendeleo ya Vijana inaongozwa na falsafa ya:

1. **Kufanya kazi kwa kasi**,
2. **Viongozi kufikika**, na
3. **Matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma kwa vijana**.

Katika kutekeleza falsafa hiyo, Wizara imeanzisha **Dawati la Huduma kwa Wateja** ambalo limekuwa likipokea kero, changamoto na maoni kutoka kwa vijana mbalimbali nchini. Kupitia dawati hilo, vijana wamekuwa wakieleza changamoto wanazokabiliana nazo, na Wizara imekuwa ikiwasaidia kwa kuwaunganisha moja kwa moja na **Maafisa Maendeleo ya Vijana katika mikoa na halmashauri zao** ili wapate msaada na fursa zinazopatikana katika maeneo yao.

**Ndugu vijana,**

Ni muhimu pia kuelewa tofauti kati ya **Jukwaa la Vijana (Vijana Platform)** na **Baraza la Vijana** ili kuelewa dhamira ya Serikali kuwa na vyombo hivi viwili. Jukwaa la Vijana (Vijana Platform) ni mfumo mpana wa ushiriki wa vijana unaolenga:

- Kuwafikia vijana wengi zaidi katika makundi mbalimbali,
- Kusikiliza maoni, changamoto na mapendekezo yao,
- Kuwapa taarifa za fursa na huduma,
- Na kuwaunganisha na Serikali na Wadau wa Maendeleo.

Kwa upande mwingine, Baraza la Vijana ni chombo rasmi cha uwakilishi wa vijana chenye majukumu ya:

- Kuwakilisha maslahi ya vijana katika ngazi za maamuzi,
- Kuratibu shughuli za mashirika na makundi ya vijana,
- Kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu masuala ya vijana,
- Na kusimamia ajenda za maendeleo ya vijana kwa mtazamo wa kitaasisi.

Hivyo basi:

- **Jukwaa la Vijana** linahusu ushiriki mpana na mawasiliano ya moja kwa moja na vijana wengi bila kujali itikadi zao za kisiasa, dini, kabila, maeneo watokayo, rangi au hali waliyonayo.
- **Baraza la Vijana** linahusu uwakilishi rasmi na uratibu wa masuala ya vijana katika ngazi za kitaasisi kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Taifa.

Vyombo hivi viwili vinakamilishana, na vinaonesha dhamira ya Serikali ya kuhakikisha vijana wanapata nafasi ya kushiriki moja kwa moja, lakini pia wanakuwa na chombo rasmi cha uwakilishi katika masuala yanayowahusu.

**Ndugu vijana,**

Kupitia Jukwaa hili la Vijana wa Vyuo Vikuu, Wizara imeanzisha pia **shindano la uandishi wa wazo bora la biashara**. Lengo la shindano hili ni kuwahamasisha vijana mnapohitimu elimu ya vyuo kuwa na mawazo bora ya biashara yanayotekelezeka na yanayoweza kuongeza fursa za ajira.

Katika shindano hili:

- Washindi watano wataibuka na kupatiwa zawadi ya fedha ili waanze kutekeleza mawazo yao ya biashara.

- Mchakato wa kuchakata na kuchambua mawazo ya biashara utafanywa na wataalamu bobezi walioteuliwa mahsusi, ili kuhakikisha ushindani unakuwa wa haki na wenye weledi mkubwa.
- Vilevile, vijana mtapatiwa elimu na maarifa kuhusu fursa mbalimbali zinazotengenezwa na Serikali kupitia taasisi zake.

Napenda pia kuwafahamisha kwamba zawadi kwa washindi zitakabidhiwa leo hii**,** ili waanze mara moja utekelezaji wa mawazo yao ya biashara.

**Ndugu vijana,**

Kupitia Vijana Platform, tunataka:

- Kusikia sauti zenu,
- Kujifunza kutoka kwenu,
- Kushirikiana nanyi katika kubuni suluhisho,
- Na kuwawezesha kutimiza ndoto zenu.

Huu ni mpango wenu. Mafanikio yake yatategemea ushiriki wenu, nidhamu yenu, na ari yenu ya kujituma.

Kabla ya kuhitimisha hotuba yangu ninaomba kuwahimiza vijana wote kutumia jukwaa hili kikamilifu. Jiungeni, shiriki mijadala, toeni mawazo, anzisheni miradi, na tumieni fursa zinazotolewa na Serikali. Serikali ipo pamoja nanyi, na mustakabali wa Tanzania upo mikononi mwenu. Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu ninaomba kumshukuru Mkuu wa Mkoa wa Singida na timu yake ya Mkoa, Mkuu wa Chuo cha TIA Singida na Vyuo vyote vilivyoshiriki pamoja na Wadau Wote waliochangia katika kufanikisha tukio hili ambalo limefana sana. Lakini pia ninatambua na

kumpongeza Afisa Maendeleo ya Vijana wa Mkoa wa Singida kwa Uratibu mzuri wa shughuli za Maendeleo ya Vijana. **Hongereni sana.**

Baada ya kusema hayo machache, nanatamka Vijana Platform kwa Vijana wa Vyuo Vikuu na Vya Kati Mkoani Singida limefunguliwa Rasmi,

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**
**Mungu ibariki Tanzania.**
**Mungu awabariki vijana wa Tanzania.**